Toleo Nam. 002/ Februari 2020 / Haliuzwi

# ZURA

ZURA
Zanzibar Utilities Regulatory Authority

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar



## ZURA Kujivunia ofisi ya kisasa Uk. 4

## ZECO yazidi kuing'arisha Zanzibar Uk. 14

Email:info@zura.go.tz / Facebook: zura / Instagram:zura_mamlaka / Twitter:zura_znz / Website:www.zura.go.tz

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu:**
Dk. Ally S. Mwinyikai

**Msaidizi Mhariri Mkuu:**
Khatib H. Khatib

**Waandishi:**
Khuzaimat Bakar Kheir
Mbarak Hassan Haji
Hassan Juma Amour

**Mpiga Picha:**
Hassan Juma Amour

**Msanifu:**
Aziz Iddi Suwedi

**Msambazaji:**
Mwinyi Ahmed Mwinyi

## Daraja la Mawasiliano

Hili ni toleo la pili la Jarida la ZURA lililoandaliwa kwa lengo la kuwapa nafasi wananchi kufahamu majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, Zanzibar (ZURA) na utekelezaji wa kazi zake za kila siku.

Katika shughuli zake za kila siku, ZURA imekuwa ikijihusisha na sekta ya maji, mafuta, umeme na gesi, mambo ambayo yana umuhimu makubwa katika maisha ya kila siku ya binadamu. Kutolewa kwa Jarida hili ni kutaka kupata ushirikiano kutoka kwa wananchi kwa dhamira ya kukuza na kuendeleza ustawi na maendeleo ya jamii kwa faida ya wananchi na Taifa kwa jumla.

Kinachotakiwa ni wananchi kutoa mawazo, fikra na michango yao kwenye Jarida hili kwa mtindo wa Makala, habari, picha na maoni. Makusudio ni kulifanya jarida hili kuendelea kuwa daraja madhubuti la kuwaunganisha wananchi na Mamlaka kwa sasa na siku zijazo.

Uongozi wa ZURA unaamini kwamba kuendelea kwa Jarida la ZURA, kutategemea sana mawazo, fikra, maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau kupitia njia tofauti za mawasiliano kutoka sehemu mbalimbali za Zanzibar.

Hadi hivi sasa, bado sio wananchi wengi waliojitokeza kutoa michango yao ambayo itakapopatikana itakuwa ikichapishwa kwenye majarida yajayo. Michango itakayotolewa na wadau ni moja miongoni mwa njia zitakazotumiwa na Mamlaka kupata mrejesho wa huduma zinazotolewa na hivyo kuweza kujitathmini.

Kwa ajili ya kuwasiliana wadau wanaweza kutumia:

P.O. Box 2238
Zanzibar- Tanzania
Simu: +255 24 223 8316
Eax: +255 24 223 8317
Email: info@zura.go.tz

## MAONI YA MHARIRI

# Wananchi ungeni mkono juhudi za Serikali

**SERIKALI** ya Mapinduzi Zanzibar imefanya kazi kubwa ya kuwapatia wananchi wake wa mjini na vijijini huduma zote muhimu za jamii ikiwemo maji safi na salama.

Maji ni huduma muhimu sana siyo tu kwa maisha ya mwanadamu, lakini vile vile kwa viumbe wote, miti na mimea. Wapo waandishi na wanasanaa kadhaa walioandika na kuimba wakielezea umuhimu wa maji na kwamba iwapo yataadimika, basi kwa kweli viumbe wataishi katika maisha ya shida sana.

Huduma hii ya maji ina umuhimu wa kipekee katika kuwaendeleza wananchi kiuchumi, na hasa wakati huu ambapo teknolojia inaendelea kukua kwa kasi kubwa. Kwa mfano kilimo cha kisasa cha umwagiliaji maji kimeonesha mafanikio makubwa katika miaka ya hivi karibuni na wakulima wengi wamejielekeza kwenye kilimo hicho kinachohitaji maji mengi lakini chenye tija kubwa.

Kutokana na umuhimu wake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kugharamia Mradi wa Maji safi na salama katika Mkoa wa Mjini/Magharibi, ambao ulihusisha mambo mbali mbali yenye mnasaba na huduma hiyo ikiwemo uchimbaji wa visima vipya sita (6), vyenye uwezo wa kuzalisha wastani wa lita 150,000 kwa saa kwa kila kisima kimoja, kuvihuisha visima vikongwe 23 na kujenga matangi mawili (2) mapya huko Saateni na Mnara wa Mbao, yenye ujazo wa jumla ya lita 3,000,000.

Mradi huu uliogharimu jumla ya shilingi Bilioni 37.142 una lengo la kuondosha kabisa kero ya muda mrefu ya upatikanaji wa huduma hiyo, ambayo imekuwa ikiwakabili wananchi wa Mkoa wa Mjini/Magharibi. Kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu wa mradi huo, wananchi wapatao 283,198 wa Mjini wanaoishi katika Shehia 27 zilizoko wilaya ya Mjini, watafaidika na mradi huo.

Kukamilika kwa mradi huo ni hatua yenye kuleta matumaini na ni faraja kubwa miongoni mwa wananchi wanaokwenda na wakati. Ni ukweli ulio wazi kwamba wapo miongoni mwa wanajamii ambao wanashindwa kuiona neema hiyo na hivyo kutoithamini na kushindwa kuitumia ipasavyo kwa kutengeneza mambo muhimu katika maisha yao kama vile ajira binafsi.

Mradi huu sio wa kwanza kutekelezwa na Serikali katika uhuishaji wa sekta ya maji nchini. Awamu zote zilizopita za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimetekeleza miradi ya aina hiyo yenye kuleta matumaini. Kwa bahati mbaya, kutokana na sababu tofauti malengo yaliyokusudiwa bado hayajafikiwa.

Upo ushahidi wa wazi unaothibitisha kuwa juhudi hizo za Serikali za kusambaza maji sehemu zote, zimekuwa zikikwamishwa na baadhi ya watendaji ambao wanashindwa kuwajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao ya kudhibiti miundo mbinu na uharibifu wa vyanzo vya maji unaosababisha kupungua na hata kukauka kwa maji katika baadhi ya vyanzo hivyo.

Tumewataja watendaji wa taasisi zinazosambaza maji kwa sababu tu, wao ndio wenye jukumu la kusimamia huduma hizo. Hata hivyo, waharibifu wakubwa wa miundo mbinu na wanaoondoa udhibiti wa vyanzo vya maji ni wananchi wenyewe wanaotanguliza mbele maslahi yao binafsi kuliko maslahi ya Taifa.

Ifahamike wazi kwamba, kukosekana kwa maji safi na salama ndio chanzo cha matatizo mengi katika jamii ikiwemo kuibuka miripuko ya magojwa, kusimama kazi zinazohusu matumizi ya maji majumbani, kwenye kilimo, viwandani na hata shughuli nyengine za kiuchumi na kijamii.

Zanzibar iliyodhamiria kweli kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii inahitaji uhakika wa maji kwa wananchi wake na katika maeneo yote ya uzalishaji. Hili linawezekana iwapo tu kila mtu ataunga mkono juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo ya Taifa na wananchi wake kwa jumla.

# Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu ZURA



**Bw. Haji Kali Haji -** Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, Zanzibar (ZURA)

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), sina budi kuwatakia salaam za kheri na fanaka za mwaka mpya 2020 wasomaji wa Jarida hili.

Kwa kuwa huu ni mwanzo wa mwaka sina budi kuwaeleza wasomaji wa Jarida hili pamoja na Wananchi wote kwamba Mamlaka imejiandaa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa zaidi ndani ya mwaka huu wa 2020.

Kwa ajili ya kutimiza malengo yake, wananchi watarajie ndani ya mwaka huu kuendelea kunufaika na mafanikio yatakayoletwa na ZURA katika sekta zote muhimu zinazosimamiwa na ZURA ambazo ni Maji, Umeme, Mafuta na Gesi ya Kupikia .

Wananchi ndani ya kipindi hichi cha mwaka 2020 watarajie kuanza kutumia Majengo mapya yaliyojegwa na Mamlaka. Majengo hayo yako katika eneo la Maisara Mkabala na Makataba Kuu ya Zanzibar, ambayo yanatarajiwa kufunguliwa mwezi Aprili 2020. Kuhamia katika jengo hilo kutaweka mazingira bora zaidi ya kufanya kazi kwa wafanyakazi wa Mamlaka pamoja na Wizara lakini pia yataimarisha lengo la Serikali la utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mbali na mafanikio hayo, wananchi watarajie kuona mafanikio mengine ya Ujenzi wa Bandari na Bohari mpya ya kuhifadhia mafuta itakayojengwa Mangapwani/Bumbwini. Ujenzi wa bandari hiyo unatarajiwa kuanza rasmi mwishoni mwa mwaka huu ambao utakuwa na awamu mbili. Awamu ya kwanza itaanzisha ujenzi wa matangi yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta lita milioni 30 ambayo sawa na matumizi ya miezi miwili, hivyo kutakuwa na akiba ya kutosha. Ujenzi huo utakapokamilika utakuwa ni kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wa nchi na kuleta mapato kwa Serikali.

Aidha, matayarisho ya ujenzi wa Bandari hiyo yanaendelea na hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kukamilika ulipaji fidia kwa vipando na mali za wananchi wa eneo hilo. Pia, ujenzi wa nyumba 31 za wananchi (katika kijiji cha Dundua) ambao watalazimika kuhama ili kupisha mradi umefikia asilimia 90 na unatarajiwa kukamilika mwezi machi, 2020. Wananchi hao wataanza kunufaika na maisha yao mapya kwani mbali na kuishi katika nyumba zao hizo walizojengewa watanufaika pia na huduma za Skuli, Msikiti, Hospitali pamoja na maduka. kwa jumla eneo hilo la Dundua litakuwa ni eneo la mji mpya wa kisasa.

Kwa upande wa upembuzi yakinifu (Feasibility Study) kwa ajili ya mradi huo, matayarisho yake yameshaanza ambapo upembuzi huo utagharamiwa na mkopo wa Benki ya Exim ya Afrika.

Katika toleo letu la kwanza la Jarida la ZURA tulielezea mpango wa Mamlaka wa kuanza kutoa leseni kwa wafanyabiashara wa gesi ya kupikia majumbani. Mpango huo utaanza rasmi katika kipindi hiki ambapo wauza gesi wote watatakiwa kukata leseni zao kupitia kuwa ZURA. Mpango huo wa utoaji leseni za gesi utasaidia kudhibiti upandaji wa bei za Gesi kiholela na pia kuimarisha ukuaji wa biashara hiyo ambayo inaonekana kuwa ni chanzo cha kuimarisha mazingira safi na salama.

Katika kuhakikisha ZURA inatekeleza majukumu yake ya kuwajali wananchi katika matumizi ya Umeme, itaanza kwa mara ya kwanza kutoa leseni kwa Shirika la Umeme la Zanzibar ZECO ambayo itapaswa kukata leseni hiyo hivi karibuni.

Faida ya ZECO kupatiwa leseni kutoka ZURA itasaidia kuweza kudhibiti na kuisimamia vyema sekta hiyo na pia kuhakikisha kuwa Shirika hilo halipandishi bei zake kiholela.

# ZURA kujivunia ofisi ya kisasa



Muonekano wa Jengo jipya la ZURA liliopo Maisara Jijini Zanzibar likiwa katika hatua za mwisho wa ujenzi wake

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) hivi karibuni inatarajia kuzindua rasmi jengo lake jipya lenye ofisi za kisasa zenye kulingana na hadhi ya Mamlaka hiyo.

Jengo hilo ambalo lina ghorofa sita (6), liko katika eneo la Maisara, karibu na jengo la Maktaba Kuu, Zanzibar, hivi sasa liko katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wake.

Ujenzi wa ofisi hizo za ZURA unakwenda sambamba na ujenzi wa ofisi za Wizara inayosimamia shughuli za ZURA ikiwa ni miongoni mwa mafanikio makubwa ya utekelezaji wa mipango ya Serikali ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein.

Miongoni mwa mafanikio makubwa aliyoyapata Rais Shein ni kuzipatia ofisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar majengo yenye hadhi kwa kujenga majengo mengi ya ofisi za Serikali na kuacha kutumia majengo yaliyorithiwa kutoka enzi za ukoloni au nyumba za kuishi ambazo mara baada ya Mapinduzi ya Januari, 1964 zilitaifishwa na kuwa mali ya Serikali.

Ujenzi wa majengo ya ofisi za kisasa ni sehemu ya kuendeleza kasi iliyoanzishwa na nchi za ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ya kusimamisha majengo yenye hadhi yanayotumiwa na ofisi za Serikali. Majengo hayo pia yanabeba dhana nzima ya Serikali ya kuanzisha miji mipya yenye kutoa haiba nzuri ya kisasa.

Chini ya mpango huo, ZURA hivi karibuni itafaidika kuwa na majengo ya uhakika itakayoyatumia kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa na taifa. ZURA ina majukumu makubwa ya kiutendaji kwa kuwa inashika dhamana nyeti kwa ajili ya maendeleo ya taifa ya udhibiti wa huduma za maji na nishati.

Kuanza kutumia majengo hayo, Zanzibar itajijengea heshima kubwa pamoja na Mamlaka kwa kuwa na ofisi za kisasa zinazolingana na hadhi na utendaji kazi wa kila siku kwa taasisi kubwa kama ZURA.

Kwa ofisi hizo ZURA itaondoakana na unyonge wa kutafuta maeneo ya kukutana na matajiri wakubwa kutoka nje wenye makampuni makubwa na hivyo kujivunia kuwa na ofisi zenye kumbi za mikutano yenye hadhi ya kuwakutanisha matajiri wenye hadhi kubwa kama waendesha biashara ya mafuta na gesi duniani.

ZURA ikiwa ni mwanachama wa Jumuiya ya Wadhibiti wa Nishati kwa nchi za Afrika Mashariki, kwa kuwa na jengo hilo haitokuwa na wasiwasi wa kuandaa mikutano na makongamano mbali mbali inayozikutanisha nchi hizo wanachama.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein akiondoa pazia kuashiria kuzindua Mradi wa Maji Safi na Salama na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mjini/Magharibi Unguja katika eneo la Saateni, Jijini Zanzibar

# Zanzibar yafanikiwa kusambaza maji safi, salama

Mafanikio ya juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji wa maji safi na salama katika eneo la Mjini Unguja yameanza kuonekana baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kuzindua Mradi mkubwa wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Mkoa wa Mjini/Magharibi (ZUWSP)-ADF 12 huko Saateni Wilaya ya Mjini Unguja katika shamrashamra za kusherehekea miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Si muda mrefu ujao, changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji wa huduma ya Maji safi na salama katika Mkoa wa Mjini/ Magharibi itabaki kuwa ni historia", alisema Rais wa Zanzibar katika hotuba yake wakati wa ufunguzi wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Hatua hiyo imebainisha mafanikio mengine ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya Awamu ya Saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein ambayo imepata sifa nyingi siyo tu kwa mikakati yake kabambe ya kuimarisha miradi ya maji safi na salama, lakini vile vile kwa miradi mingine kadhaa kama vile miradi ya usambazaji umeme vijijini na hasa kwenye visiwa vidogo, na mipango yake ya upatikanaji wa mafuta na gesi asilia.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa (ZAWA) Nd. Mussa Ramadhani Haji akitoa maelezo ya Kitaalamu ya ujenzi wa Tangi la Maji Saateni Zanzibar, wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi huo wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira

Katika hotuba yake hiyo ambayo pia ilirushwa moja kwa moja kupitia vyombo mbali mbali vya habari na mitandao ya kijamii, Dk. Shein alisema kuwa huduma za maji safi na salama kabla ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 zilikuwa zikitolewa kwa ubaguzi licha ya kuwa ni neema aliyoileta Mwenyezi Mungu kwa waja wake.

Akizungumzia umuhimu wa maji kwa wanaadamu, wanyama na miti, Rais wa Zanzibar amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa huduma hiyo inaimarika, kwani amesema huduma ya maji haina mbadala kwa binadamu na viumbe wote hai.

Aidha, Dk. Shein alieleza jinsi Washirika wa Maendeleo ikiwemo Ras Al - Khaimah, Sharja, Japan, China, India na wengineo walivyoiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha miradi ya maji safi na salama hapa nchini.

Kumbukumbu katika nyaraka mbali mbali zinaonesha kuwa Zanzibar ina historia kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama. Kwa mujibu wa kumbukumbu hizo Zanzibar ilikuwa kituo kikuu ambapo meli maalum kutoka nchi za nje zilikuwa zikija kutia nanga na kuchukua maji kutokana na sifa za maji ya Zanzibar.

Hata hivyo, kutokana na kasi kubwa ya ongezeko la watu, kumetokea uhaba wa maji hapa Zanzibar na hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulazimika kutafuta fedha kwa ajili ya kuimarisha miradi ya maji katika eneo la mji wa Zanzibar na hatimaye kupatikana kwa kiasi cha dola za Marekani Milioni 268 kwa ajili ya miradi hiyo.

Azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea baada ya Mapinduzi ni kuhakikisha kiwango cha maji kinaongezeka sambamba na kasi ya ongezeko la idadi ya watu ili wananchi waweze kupata huduma hiyo ipasavyo. Katika kufikia lengo hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein, imetekeleza malengo ya Mapinduzi sambamba na Utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa vitendo.

Rais wa Zanzibar alimpongeza Waziri wa Wizara hiyo kwa kuiongoza Wizara pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hiyo kwa kushirikiana, “Namie kidogo nimeubwaga moyo katika kufanikisha mradi huu wa maji”alisema Rais Dk. Shein katika hotuba yake hiyo.

Rais wa Zanzibar alitumia fursa hiyo kuelezea historia ya Mapinduzi hapa Zanzibar

na jinsi jitihada za makusudi zilivyochukuliwa katika kuhakikisha ukoloni unaondoshwa na wananchi wa Zanzibar wanaishi maisha bora na wanaondokana na dhulma iliyokuwepo.

Alieleza kuwa Mapinduzi yaliyofanyika Januari 12, 1964 ni Mapinduzi halali na lengo lake ni kuhakikisha wananchi wanaishi maisha bora ya amani sambamba na furaha na kushirikiana, hatua ambayo ilipelekea nchi kadhaa duniani kuyatambua.

Aliwanasihi wananchi na kueleza kuwa si busara na wala si vizuri wakaunganisha maji katika nyumba zao bila ya kufuata sheria na utaratibu uliowekwa.

Alisisitiza kuwa Zanzibar maji hayalipiwi bali yanachangiwa katika kupatikana kwa huduma hiyo na kuwataka wananchi pale Serikali inapowaelekeza kuchagia huduma hiyo basi wasirudi nyuma kwani hatua hiyo itaisaidia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kufikisha na kutengeneza miundombinu ya maji kwani ina lengo na nia nzuri huku akisisitiza haja ya kutunzwa kwa miundombinu hiyo ya maji.

Aliendelea kusisitiza haja ya kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji kwani hivi sasa vimekuwa vikivamiwa kwa kujengwa nyumba katika maeneo hayo likiwemo eneo la Mwanyanya huku akisisitiza umuhimu wa kupandwa miti na kukemea kukatwa miti ovyo.

Aidha, Dk. Shein aliitaka ZAWA kuwa na wataalamu wa maji kutokana na kuwepo kwa miundombinu mipya ya maji hivi sasa, hivyo ni lazima wajiandae kuwapa elimu na mafunzo watendaji wake katika vyuo kadhaa vikiwemo vya ndani na nje ya nchi vinavyosomesha kada hiyo.

Aliwataka wafanyakazi wa ZAWA kutofanya kazi kwa mazoea na kusistiza kuwa ni vyema wakawepo watu wenye utaalamu wa kutosha katika kada hiyo ili kupelekea ufanikishaji wa utoaji wa huduma ya uhakika wa maji safi na salama.

Rais wa Zanzibar alisisitiza haja ya kuwepo kwa hakiba ya vifaa katika Mamlaka ya ZAWA ili kuepuka uhaba wa vifaa pamoja na kuwepo timu kabambe ya kufuatilia matatizo ama uvujaji wa ovyo wa maji na sio kutegemea taarifa kutoka kwa wananchi.

Alisisitiza haja ya kuwaajiri vijana ili wafanye kazi kwani wako wengi hawana kazi ili lengo la kufanikisha utoaji wa huduma hiyo lifikiwe.

Alitumia fursa hiyo kumpongeza Mkurugenzi wa ZAWA, Bw. Mussa Ramadhan Haji na timu yake kwa hatua anazozichukua hasa wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa kuwapelekea maji wananchi katika mwezi huo mtukufu na kuwataka waendelee na utaratibu huo.

Aidha, aliipongeza Serikali ya Japan kwa kusaidia hatua ya mwanzo ya mradi wa maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kuendelea kutoa msaada wake ikiwemo pale Serikali inapotaka kukopa, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambao wameanza kusaidia tokea mwaka 1964 pamoja na Serikali ya India.



Moja kati ya picha inayoonesha namna mabomba ya maji safi na salama yalivyosambazwa katika jiji la Zanzibar

# 283,198 wanufaika na Mradi wa Maji Mjini



Tangi la Maji safi na Salama liliopo Saateni Unguja lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita Milioni mbili

Wananchi wapatao 283,198 wanaoishi katika Shehia 27 za Mji Mkongwe na Ng'ambo ya zamani wanatarajiwa kunufaika na mradi wa Maji safi na Salama ambao umetekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mradi huo ulioanza rasmi mwezi Julai 2013 na kukamilika mwezi Disemba 2019.

Akizungumza katika sherehe za ufunguzi wa Mradi huo, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati Ali Khalil Mirza amesema Mradi huo hadi kukamilika kwake umegharimu jumla ya TZS Bilioni 37.142, ambapo kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa TZS Bilioni 3.809 na Benki ya Maendeleo ya Afrika imetoa TZS Bilioni 33.332. Tangi la Saateni limegharimu jumla ya TZS Bilioni 2.937 na kwa upande wa tangi la Mnara wa Mbao limegharimu TZS Milioni 908.536.

Shehia zitakazonufaika na mradi huo ni Shangani, Mkunazini, Kiponda, Malindi, Mchangani, Vikokotoni, Mwembetanga na Kisiwandui. Nyengine ni Kikwajuni Bondeni, Kikwajuni Juu, Kisima Majongoo, Mlandege, Mwembeladu, Rahaleo, Mikunguni na Mkele. Vile vile shehia za Mwembeshauri, Shaurimoyo, Mwembe Makumbi, Kwaalamsha, Gulioni, Miembeni, Kilimani, Kwahani, Kwaalinato, Makadara na Migombani nazo zitanufaika kwa kupata maji safi na salama.

Kwa mujibu wa maelezo ya Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, mradi huo umesimamiwa na Mshauri Mwelekezi kutoka Kampuni ya Don Consult Ltd na ujenzi wa matangi na ulazaji wa mabomba umefanywa na Mkandarasi kutoka Kampuni ya Stcol Corporation. Uchimbaji na ukarabarti wa visima umefanywa na Kampuni ya NSPT Ltd.

Mradi umejumuisha uchimbaji wa visima sita (6) vipya vyenye uwezo wa kuzalisha wastani wa lita 150,000 kwa saa kwa kila kisima, ukarabati wa visima vikongwe 23, ujenzi wa matangi 2 yenye ujazo wa lita milioni mbili (2) Saateni na milioni moja (1) Mnara wa Mbao.

Aidha, mradi huo unajumuisha ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 75.7 ambapo kilomita 20.6 ni mabomba ya usafirishaji maji yenye kipenyo kuanzia inchi 12 hadi 24 yaliyolazwa kutoka visimani Bubwisudi hadi Welezo Matangini na kutoka visimani Kaburi Kikombe hadi tangi la Mnara wa Mbao.

Katibu Mkuu huyo alisema kuwa baada ya kukamilika kwa mradi, uzalishaji wa maji katika visima 23 vilivyofanyiwa marekebisho umeongezeka kutoka lita Milioni 32.789 hadi kufikia lita milioni 36.755 sawa na ongezeko la asilimia 12.

Visima vipya sita (6) kwa sasa vinazalisha lita milioni 22.550 hivyo kufanya jumla ya lita zote hizo kwa siku kuwa ni milioni 59.305 sawa na ongezeko la asilimia 36. Uzalishaji huo unatarajiwa kuwanufaisha wakaazi wapatao 283,000 na kwamba uzalishaji huo unatarajiwa kuwa endelevu.

Miradi mengine iliyobuniwa na inayotegemewa kutekelezwa katika kipindi cha karibuni ni pamoja na Mradi wa Uhuishaji wa Mfumo wa Usambazaji maji Zanzibar, Mradi wa Uhuishaji wa Huduma za Usambaji Maji Safi wa Mazingira

Miji 26 ya Tanzania ikiwemo Zanzibar na Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini/Magharibi yenye gharama za Dola za Kimarekani 247.

Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati Mhe. Salama Aboud Talib alieleza kuwa hatua hizo zote zinalenga katika kuhakikisha kuwa lengo, madhumuni na dhamira ya Dk. Ali Mohamed Shein ya kuhakikisha kuwa wananchi wa Mjini Unguja na Zanzibar kwa jumla wanaondokana na usumbufu wa upatikanaji wa huduma hiyo muhimu zinafikiwa.

Alisema kuwa jitihada hiyo ni matokeo ya jitihada za pamoja na ushirikiano miongoni mwa wahusika wote katika utekelezaji wa mradi huo.

Alieleza kuwa Zanzibar imekuwa nchi ya kwanza miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki kujenga matangi ya maji ya aina hiyo na kupongeza jitihada za Rais Dk. Shein kwa kazi hiyo kubwa ya mradi huo iliyofanyika ya kuhakikisha kuwa huduma ya maji inaimarika katika mji wa Zanzibar.

Aliwapogeza viongozi waliokuwa wakitoa mashirikiano katika kuhakikisha kuwa mradi huo unafanikiwa wakiwemo Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi Hassan Khatib Hassan, Masheha wa Mkoa huo ambao wamefanya kazi kubwa katika kusimamia miradi hiyo na kupelekea kufanya kazi bila ya bughudha katika kufanikisha mradi huo.

Sambamba na hayo, Waziri huyo alikipongeza Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kusimamia Ilani ya chama hicho kwa kuweza kusaidia kufanikisha mradi huo ikiwa ni pamoja na ziara mbali mbali walizozifanya wakati wa ujenzi wa mradi huo.

Akisoma taarifa ya kitaalamu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Ali Halil Mirza aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Shein kwa uongozi wake mahiri kwa kuamua kutekeleza Mradi wa Maji na Usafi wa Maziringira wa Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Alisema kuwa uamuzi huo ulikuwa ni wa busara na wa msingi katika kuondosha kero zinazowakabili wananchi, unaokwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM 2015-2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA III), Dira ya Maendeleo ya 2020 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), katika kuimarisha huduma za maji safi na salama Zanzibar.



Harakati za ulazaji wa mabomba ya maji safi na salama maeneo mbali mbali ya jiji la Zanzibar ambapo mradi huu utawaondolea shida ya maji wananchi wa mji huu

# Mafanikio ya Kuimarisha vituo vya Mafuta

Kuwepo kwa Mamlaka ya udhibiti wa huduma za Maji na Nishati (ZURA) kisiwani Pemba, kumesaidia uimarishaji wa miundombinu ya mafuta haswa vituo vya kuuzia mafuta kutoka katika hali mbaya vilivyokuwa mwanzo na kuwa katika hali bora zaidi na iliyo salama hivi sasa.




Muonekano wa kituo cha mafuta cha Tibirinzi baada ya marekebisho




Kituo cha Bakari Petrol Station kikionekana baada ya marekebisho




Kituo cha Bakari Petrol Station kikionekana kabla ya marekebisho




Kituo cha Chake Petrol Station kikionekana baada ya marekebisho




Kituo cha Chake Petrol Station kikionekana kabla ya marekebisho



Kituo cha Sharif Petrol Station kikionekana baada ya marekebisho




Kituo cha Chake Petrol Station kikionekana kabla ya marekebisho

## Muamko juu ya biashara ya Mafuta kisiwani Pemba

Kutokana na kasi kubwa ya ongezeko la mahitaji ya mafuta kisiwani Pemba, ZURA kupitia vipindi mbali mbali vya redio na Televisheni imeendelea kuwahamasisha wawekezaji kuwekeza zaidi kwenye sekta hiyo na hivyo kufanikiwa kupokea maombi mengi ya ujenzi wa vituo vipya. Aidha, viko vituo vipya vinaendelea kujengwa.




Kituo Kipya cha Kinyasini



Kituo Kipya cha Madenjani



Kituo Kipya cha Tumbe

## Utoaji wa mafunzo kwa wananchi pamoja na wadau wa Mafuta wa Pemba juu ya kazi za ZURA

Kutokana na Taasisi kuwa changa na Wananchi wengi kukosa kujua kazi za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), Taasisi imeweka jitihada za kuwafikia wananchi na kuwaelimisha kupitia katika matamasha mbali mbali, semina elekezi, pamoja na kwenye vyombo vya habari vya Kisiwani Pemba




ZURA ikishiriki katika maonesho ya siku ya chakula duniani yaliyofanyika Chamanangwe, Wilaya ya Wete, Pemba.



Semina elekezi iliyoandaliwa na ZURA kwa wadau wa Mafuta wa kisiwani Pemba

## Kudhibiti magendo

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) kupitia tawi lake la Pemba wakisaidiana na vyombo vya ulinzi na usalama vya Pemba imefanikiwa mara tatu (3) kukamata magendo ya Mafuta ya dizeli ndani ya mwaka mmoja. Mafuta yaliyokamatwa ni lita 7000, lita 1000 na lita 340 na kufanya jumla ya lita zilizokamatwa kuwa 8340



Lita 7000 dizeli (Kinyasini)




Lita 1000 dizeli (Mkoani)

# Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)


Ewe Mwananchi kwa matatizo yote ya umeme kama vile nguzo mbovu, kukosa umeme, mita yako kutokufanya kazi au kuharibika, kuchelewa kupatiwa huduma ya kupimiwa na matatizo mengine yanayohusu huduma zetu hakikisha unawasilisha matatizo yako ZECO wakati wowote ndani ya saa 24 kwa kupiga simu 0772877879 au 0242230232 utasikilizwa na kuhudumiwa bila ya wewe kufika katika ofisi zetu. Toa taarifa sahihi ili uhudumiwe kwa haraka.



**ZECO** tupo kung'arisha maisha yako



# ZECO yazidi kuing'arisha Zanzibar



Azma ya kusambaza umeme kwa wananchi wote imezidi kufanikiwa kutokana na Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) kutimiza kwa kiwango kikubwa malengo iliyojipangia.

Katika kutekeleza malengo yake, ZECO limefanikiwa kuwasambazia umeme wananchi katika visiwa vya Unguja na Pemba kwa asilimia 87% na hivyo kuifanya sehemu kubwa ya vijiji nchini kupata huduma hiyo muhimu kwa maendeleo.

Akizungumzia hatua zilizofikiwa na Shirika hilo, Meneja Mkuu wa ZECO, Hassan Ali Mbarouk, amefahamisha kuwa kazi ya usambazaji umeme ni endelevu. Hadi sasa mafanikio makubwa yameshapatikana kutokana na

huduma hiyo kusambaa katika maeneo yote ya mjini na vijijini, Unguja na Pemba.

Amesema jambo la kujivunia ni kuwa shehia zote za Unguja na Pemba zimefikishiwa huduma ya umeme na vijiji vyote vikubwa vinapata huduma ya umeme isipokuwa vitongoji vichache na maeneo mapya yanayochipuka hivi sasa.

Meneja Mkuu huyo alifahamisha kuwa visiwa vidogo vidogo vinane (8) kati ya 10 wanavyoishi watu tayari vimeshapatiwa huduma ya umeme Unguja na Pemba na visiwa viwili vilivyobakia vinatarajiwa kupatiwa huduma hiyo ndani ya mwaka huu wa 2020.

Ameeleza kuwa kazi yote ya usambazaji umeme inafanywa na Serikali kupitia Shirika lake la Umeme na kwamba hivi sasa inaratibu maeneo mapya ya makazi na kilimo ili yaweze kuwekwa katika mpango kazi wake wa kuyapelekea umeme.

Amefahamisha kuwa kuimarika kwa sekta ya umeme nchini kumesababisha maendeleo katika nyanja nyengine za kiuchumi kama vile biashara, kilimo, Utalii na mawasiliano.

Lengo la Serikali, Meneja mkuu amesema, ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2022 vijiji vyote vinanufaika na huduma ya umeme. Hata hivyo, amesema kasi ya uungaji umeme majumbani bado haijaridhisha kwa vile hadi sasa ni asilimia 55 tu ya kaya ndio zimeunganishiwa umeme.

Hivyo, kazi kubwa inayolikabili Shirika la Umeme ni kuwahamasisha wananchi kuweza kuunganisha huduma za umeme majumbani mwao ikiwa ni sehemu muhimu ya kujiimarisha kiuchumi na kijamii.

"Katika kushajiisha wananchi kuunganishwa katika huduma ya umeme, ZECO imetoa fursa ya kuwakopesha wananchi katika uungaji wa umeme ili kuongeza kasi ya wananchi kujiunga na huduma hiyo" alifahamisha.



# Ziara ya Bodi ya ZURA Pemba



Wajumbe wa Bodi ya Pili ya Wakurugenzi ZURA wakiwa katika mkutano wa pamoja na Uongozi wa Shirika la Umeme (ZECO) Tawi la Pemba



Meneja Bohari ya GAPCO iliyopo Wesha Pemba Nd. Justice Makubi akiwaelekeza jambo Wajumbe wa Bodi ya Pili ya Wakurugenzi ZURA wakiwa wakiwa katika ziara maalumu huku Wesha Pemba



Baadhi ya Wajumbe wa Bodi ya Pili ya Wakurugenzi ZURA wakipanda juu ya Tangi la Maji Safi na Salama liliopa Taifu Wete Pemba

# Ziara ya Bodi ya ZURA Pemba



Wajumbe wa Bodi ya Pili ya Wakurugenzi ZURA wakimsikiliza Meneja wa Shirika la Umeme (ZECO) Tawi la Pemba Nd. Mohamed Juma




Bohari ya mafuta iliyopo Wesha Pemba ambayo ilitembelewa na Wajumbe wa Bodi ya Pili ya Wakurugenzi ya ZURA




Wajumbe wa Bodi ya Pili ya Wakurugenzi ZURA wakiwa chini ya Tangi la Mafuta wakipokea maelezo kutoka kwa Meneja Bohari ya GAPCO iliyopo Wesha Pemba Nd. Justice Makubi

# Matumizi sahihi ya gesi kwa usalama wako



Hali ya utumiaji wa nishati kwa wananchi wa kawaida hasa wa mijini imebadilika sana kutokana na watu wengi kuacha kutumia nishati inayotokana na kuni na makaa na badala yake kufurahia kutumia gesi ya kupikia, "Liquefied Petroleum Gas" (LPG).

Katika kipindi cha hivi karibuni, gesi imeonekana kuwa ni sekta inayokua kwa kasi kubwa, kwani wananchi wa Zanzibar wameanza kuona umuhimu na urahisi wa kutumia nishati hiyo.

Matumizi ya gesi ni nafuu ukilinganisha na gharama za makaa, yanayopatikana kwa gharama kubwa. Watu wengi wamebaini kuwa matumizi ya gesi ni bora kwa ajili ya mapishi kwani huivisha chakula kwa haraka kuliko makaa na vile vile ni rahisi katika kugharamia upatikanaji wake.

Hatua iliyofikiwa ya utumiaji wa gesi ni mafanikio ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) yenye jukumu la kudhibiti na kusimamia huduma za maji na nishati (umeme, mafuta na gesi) kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa kawida.

Matumizi ya gesi yanaonekana kuwa ni ukombozi mkubwa wa kuondoa tishio la kuendelea kutegemea misitu kuwa chanzo kikuu cha kupata nishati ya kupikia nchini. Inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 90% ya nishati iliyokuwa ikitumika nchini kwa kupikia siku za nyuma, ilitokana na miti jambo lililoashiria tishio kubwa la kuharibu mazingira kwa kuifanya nchi kugeuka kuwa jangwa.

Ukataji na uteketezaji wa misitu uliokuwa ukifanyika kwa ajili ya kupata kuni na makaa, ulikwishaathiri ubora wa misitu nchini. Misitu ilikuwa ikipotea kwa ajili ya kupatikana kuni zinazotumika zaidi vijijini na makaa yanayotumika zaidi mijini. Matumizi ya nishati ya gesi yameonekana ni suluhisho la kukabiliana na tatizo la uharibifu wa misitu.

Gesi ya LPG hupatikana baada ya kusafishwa mafuta ghafi (crude oil). Ni nishati isiyoharibu mazingira, inayopatikana kwa uhakika kwa bei nafuu na hivyo hupelekea watu wengi ulimwenguni kuitumia.

Gesi ya LPG inatafautiana kikemikali na gesi asilia (Natural Gas). Gesi asilia inaundwa na kemikali ya 'Methane' kwa kiasi kikubwa, wakati gesi ya kupikia (LPG), inaundwa na 'Propane' na 'Butane'. Gesi asilia inaweza pia kutumika kupikia, lakini gesi hii inahitaji kuwepo mtandao wa mabomba.

LPG husafirishwa na kuhifadhiwa kwenye mitungi kwa sababu ni rahisi kubadilishwa kuwa katika hali ya kumiminika. Kwa sasa, ZURA inategemea soko la Tanzania Bara kuagiza gesi ya aina hii. Kampuni

zinazofanya Biashara ya jumla, kwa bidhaa hii kwa Zanzibar kwa sasa ni V-Gas, Oryx-Gas, Oilcom, Camel Oil, na Lake Gas.

Kama zilivyo nishati nyengine, gesi nayo ni muhimu kuzingatia misingi ya usalama ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea wakati wa upokeaji, utunzaji, usafirashaji na utumiaji wake. Ili kulinda misingi hiyo, ZURA imeweka mambo maalumu ya kuzingatiwa.

Shughuli za uingizwaji, uhifadhi, usambazaji na uuzaji wa gesi ya kupikia zinatakiwa zifanywe kwa kuzingatia misingi ya usalama na viwango. Lengo ni kukidhi usalama wa watu pamoja na mali zao, afya za watu na mazingira.

**Wakati wa kununua LPG**

Mambo muhimu mnunuzi anayopaswa kuyazingatia wakati wa ununuaji wa gesi ya kupikia ni:

i. Kununua gesi kwenye maduka/sehemu zinazotambulika (zilizosajiliwa).
ii. Kuhakikisha mtungi una:-
   - Nembo ya kampuni
   - Vali (valve) ya usalama
   - Kizibo (seal) cha kampuni husika
   - Mwaka uliotengenezwa
   - Ujazo wa mtungi
iii. Kuhakikisha anapimiwa uzito wa mitungi ili kujiridhisha na ujazo wa gesi katika mtungi wakati wa kununua.

**Usafirishaji na Uhifadhi LPG**

Wakati wa usafirishaji na uhifadhi salama wa Gesi ya kupikia inahitaji kuzingatiwa mambo yafuatayo:

i. Ni lazima mitungi isafirishwe ikiwa imesimamishwa.
ii. Mitungi ihifadhiwe sehemu yenye hewa ya kutosha na pia iwe mbali na vyanzo vya moto.
iii. Mitungi ya gesi lazima itunzwe mahali ambapo si rahisi kugongwa au kuangukiwa na kitu chochote.
iv. Mtungi mtupu (ambao hauna gesi) ni lazima utunzwe sehemu isiyokuwa na joto na yenye hewa ya kutosha.

**Utunzaji LPG**

Mambo ya kuzingatia wakati wa utumiaji Gesi ya kupikia ni:

i. Hakikisha mtungi wa gesi umeunganishwa vizuri kwenye 'regulator' na 'connections' zote ziko sawa.
ii. Hakikisha mtungi na jiko la gesi vimeunganishwa vizuri kwa kutumia paipu ambayo haijajikunja na kusababisha mbinyo utakaopelekea kuharibika paipu na gesi kuvuja.
iii. Hakikisha mtungi upo chini na jiko lipo juu ya meza. Hii inasaidia tatizo likitokea gesi kuvuja kwenda chini na kuepusha gesi kukutana na moto wa jiko.
iv. Kuhakikisha kuna hewa ya kutosha (madirisha na milango yasifungwe).
v. Usiweke kitu chochote cha plastic karibu ya jiko la gesi.
vi. Hakikisha unazima jiko vizuri baada ya kutumia na kuzima 'safety valve'.
vii. Usiache chungu bila ya uangalizi, hakikisha unakuwa karibu na jiko muda wote unapokua unapika.

**Tahadhari za kuchukuliwa**

Tahadhari zinazofaa kuchukuliwa wakati wa utumiaji wa Gesi ya kupikia ni:

Endapo utagundua kuna uvujaji wa gesi zingatia yafuatayo:

a) Usiwashe jiko kama ulikuwa hujaliwasha.
b) Zima jiko kama lilikuwa linatumika.
c) Ondoa 'regulator' ya gesi iliyoko kwenye mtungi.
d) Fungua milango na madirisha kuruhusu hewa iingie eneo hilo, lakini usitumie feni la umeme.
e) Ikiwa mtungi unaendelea kuvuja, uondoe mtungi huo na uweke sehemu ambayo ni salama, mbali na mitungi mengine kama ipo.
f) Usiwashe wala usizime kifaa chochote cha umeme kwani kufanya hivyo kunaweza kusabibisha mripuko wa mara moja (spark).
g) Usitumie simu karibu na gesi.
h) Ijue harufu ya gesi ili iwe rahisi kugundua uvujaji wa gesi.

Ikitokea kumewaka moto kutokana na gesi usichukue maji kuzimia moto. Weka ndoo ya mchanga mkavu kwa ajili ya dharura ya kuzimia moto, au tumia 'Fire Extinguisher' kuzimia moto.

# NJIA RAHISI ZA KUPUNGUZA MATUMIZI YA UMEME

Mwenendo wa maisha ya binadamu na viumbe wote duniani umekuwa ukibadilika kwa kadri miaka inavyosonga mbele.

Hali ya maisha hivi sasa ni tofauti sana na miaka iliyopita. Historia inatufundisha kuwa watu wa zamani waliishi kwanza kwa kula vyakula vibichi, baadaye wakavumbua moto uliotokana na kufikicha vijiti na majani. Baadaye walivumbua moto unaotokana na vibiriti, umeme kwa kutumia waya, kuna nishati ya jua, mawimbi ya bahari, upepo na vyanzo vingine kadhaa.

Mabadiliko hayo yanatokana na jinsi watu wanavyoishi kwa kutegemea baadhi ya mambo ambayo zamani yalionekana kuwa ni ya anasa. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na matumizi ya nishati ya umeme.

Matumizi mengi kwenye nyumba za kisasa yanahusika sana na nishati ya umeme. Nyumba za sasa zinahitaji kuwa na taa, mafeni, mashine za kufulia, viyoyozi, mafriji na majiko ya umeme. Vifaa vyote vinavyotumia umeme vinafanya maisha kuwa rahisi zaidi.

Kwa kuwa vifaa vyote hivyo vinahitaji kutumia nishati ya umeme, matumizi yake yanakuja na gharama kubwa ambazo baadhi ya watu hushindwa kuzimudu na hivyo kuamua kuacha kuvitumia vifaa hivyo, licha ya kuwa vina umuhimu katika maendeleo na maisha yao ya kila siku.

Licha ya changamoto za aina hiyo, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kunufaika na huduma ya umeme, ZURA kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali zinazoshughulikia masuala ya Nishati, imekuwa ikichukua juhudi za kuwaelimisha wananchi namna bora zaidi ya kuweza kukabiliana na gharama kubwa za matumizi ya umeme, ikiwemo kushauri mambo yanayohitajika kufanywa ili kupunguza gharama hizo. Katika hatua hiyo ya kutoa ushauri, watumiaji wa umeme wana mchango mkubwa wa kutoa katika kupunguza gharama.

Badala ya kufikiria kutotumia vifaa vyenye manufaa, kila mtumiaji wa umeme anapenda kujua ni kifaa gani kinatumia umeme mkubwa nyumbani, na kutafuta njia mbadala anayoweza kupunguza gharama kubwa.

Ni lazima kufahamu kwamba kila mtu anapopunguza matumizi ya nishati ya umeme nyumbani kwake, anapunguza gharama na anajiongezea uwezo wa kutunza fedha kwa matumizi mengine. Aidha, matumizi madogo ya umeme ni sehemu muhimu ya kutunza mazingira. Ziko njia nyingi za kupunguza matumizi ya umeme nyumbani na kufurahia zaidi maisha na kupunguza gharama. Miongoni mwa njia hizo ni:

## 1. KUTUMIA VIFAA VINAVYOTUMIA UMEME MDOGO



Kuna vifaa vingi vya umeme ambavyo viko katika kiwango na ubora wa hali ya juu vinavyotumia umeme mdogo. Vifaa hivyo viko vya kila aina vimetengenezwa kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu ya kisasa. Miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na taa, pasi, feni na friji ambavyo vimetengenezwa kwa mfumo unaowezesha kutumia umeme mdogo, vinadumu kwa muda mrefu na vinatoa huduma kwa ufanisi mkubwa.

Njia muafaka ya kupunguza gharama za matumizi ya umeme ni kuchagua vifaa vinavyotumia umeme mdogo. Kwa mfano ikiwa unapendelea kutumia majiko na oven ya umeme, unaweza kuchagua kama Toster zenye Oven ambazo zinasifika kwa uwezo mzuri wa kupikia lakini pia kwa matumizi madogo ya umeme. Unaweza kupitia maduka mbali mbali yanayouza vifaa vya umeme ujionee zaidi bidhaa za umeme zenye matumizi madogo ya umeme. Vifaa vya aina hiyo vimekuwa vikitengenezwa na kubadilika ubora wake kila wakati hivyo, ni vizuri kupitia maduka hayo kila baada ya muda.

## 2. CHOMOA VIFAA KWENYE UMEME



Umeme hutumika wakati vyombo vya umeme vimeunganishwa na kuwashwa kutoka kwenye soketi. Baadhi ya vifaa kama vile vya kupashia moto "heater", pasi, birika na jiko huhitaji kuchomekwa kwenye umeme wakati wa matumizi yake. Mara nyingi, vifaa kama hivi vikiachwa katika umeme, huweza kusababisha mtiririko wa umeme kuendelea kuwepo hata kama vifaa hivyo vimezimwa. Ni vizuri kuhakikisha plagi "plug" ya vifaa vya aina hiyo vinachomolewa kabisa kutoka kwenye soketi.

Aidha, ni vizuri kuhakikisha kuwa umeme unazimwa kwenye kila chumba ambacho hakitumiki kwa wakati huo. Watu wengi husahau kuzima mafeni, televisheni, radio na kuacha vifaa kama hita, taa na pasi vikiwa katika soketi za umeme. Ni muhimu kuwa mwangalifu na kufuatilia vitu hivi ikiwa ni sehemu ya kupunguza matumizi makubwa ya gharama za umeme.

## 3. TUMIA FENI BADALA YA VIYOYOZI KUPUNGUZA JOTO



Watu wengi wanapendelea kutumia viyoyozi kwa ajili ya kupoza hali ya hewa hasa wakati wa joto. Viyoyozi vinapendwa sana hasa wakati wa majira ya joto kwa sababu vinaingiza baridi. Lakini watu wenye mpango wa kupunguza matumizi ya umeme, ni muhimu kuchagua matumizi ya feni kuliko viyoyozi kwani viyoyozi vinasifika kwa kutumia umeme mwingi, hasa kwa kuzingatia vinafanya kazi kubwa ya kupoza joto. Ili kuokoa gharama kubwa, unaweza kuwasha kiyoyozi kwa muda mchache mpaka hali ya joto itakapopoa, kisha kuendelea na matumizi ya feni ya kawaida.

Utaratibu wa kupunguza kutumia kiyoyozi kwa muda mrefu kutapelekea kuokoa gharama za umeme. Baadhi ya viyoyozi vya kisasa vina mfumo unaokiwezesha kiyoyozi chenyewe kujizima baada ya muda fulani utakaoupendelea, na kujiwasha pale joto linapoongezeka. Aina hii ya viyoyozi vina punguza gharama kubwa ya umeme. Hivyo, ni busara katika kutafuta viyoyozi kununua aina hii ya viyoyozi vyenye unafuu wa kutumia nishati ya umeme.

## 4. TUMIA NISHATI ZA UMEME MBADALA



Njia nyingine ya kupunguza gharama kubwa ya matumizi makubwa ya umeme ni kutumia njia mbadala kwa baadhi ya mambo. Miongoni mwa njia hizo ni kutumia nishati nyegine kwa baadhi ya mambo kama vile gesi asilia kwa ajili ya kupikia. Vifaa vya umeme unaotokana na jua (solar) vinaweza pia kuwa jibu la tatizo la matumizi makubwa ya umeme.

Maendeleo ya teknolojia yanaongeza kuwepo kwa vifaa vingi vinavyotumia mfumo wa jua kama vile Balbu za majumbani, feni na pasi. Vifaa hivi vinaweze kupunguza sana gharama za umeme. Japokuwa matumizi yake yanaweza kuwa na mipaka kwa kiasi fulani, lakini gharama zake ni za chini sana kuliko gharama za malipo ya umeme wa kawaida.

Nishati ya umeme unaotokana na jua ni rahisi sana na unaweza kutumika katika baadhi ya maeneo ya mijini na vijijini. Aidha, nishati hii inaweza kuwa ni mkombozi kwani mbali ya kuwa gharama zake ni nafuu, lakini inaweza kupatikana katika maeneo ya vijiji ambavyo havijaunganishwa kwenye umeme wa kawaida.

## 5. PANDA MITI



Kupanda miti pamoja na kuimarisha misitu ni eneo jengine muhimu la kuokoa gharama kubwa za umeme. Kupanda miti ni njia nzuri ya kutunza mazingira na pia ni sehemu ya kusaidia upatikanaji wa hewa nzuri ya mzunguko wa hewa na vivuli. Hivyo, unapokuwa nyumbani, badala ya mtu kufikiria kuwasha kiyoyozi na feni anaweza kutumia vivuli vya miti na hewa yake kuwa mbadala wa kupunga upepo. Kuna haja ya kujenga utaratibu wa kupanda miti karibu na nyumba za kuishi kwa kufahamu kuwa ni tegemeo la muda mrefu sana la kupunguza gharama za umeme kwa miaka mingi mbele.

Kwa jumla, zipo njia nyingine nyingi za kupunguza matumizi makubwa ya umeme majumbani. Linalofaa kuzingatiwa ni kuhakikisha njia hizo zinakuwa salama na rahisi. Njia mbadala salama na rahisi za nishati ya umeme ndio hizo za uimarishaji wa mazingira safi na utumiaji wa vifaa vyenye ubora. Njia hizo ni suluhisho katika kupunguza matumizi makubwa ya umeme.



# Umeme wa Jua unavyozuia tatizo la kukatika umeme



Asilimia kubwa ya watu wa Zanzibar hivi sasa wanatumia nishati ya umeme katika shughuli zao mbalimbali. Hutumia nishati hiyo kwa matumizi ya nyumbani ikiwemo kuwasha taa, kupikia kwa kutumia majiko ya umeme, kuendesha vifaa vya elektroniki kama television, friji na kucharge simu.

### Utumiaji wa Umeme

Matumizi haya yanaifanya huduma hii ya umeme kuwa ni muhimu na ya lazima katika maisha ya kila siku ya binadamu Zanzibar na duniani kote. Umuhimu na ulazima wa huduma hiyo Zanzibar ndio uliopelekea kuundwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

Katika udhibiti wake, ZURA inakuwepo katikati ili kuhakikisha kuwa huduma hizo zinawafikia wananchi muda wote zikiwa katika hali ya ubora na usalama kwa maisha ya binadamu na viumbe hai. Hata hivyo, baadhi ya wakati wananchi hukabiliana na changamoto katika kuendesha kazi zao hasa za kibiashara kutokana na kukosa huduma ya umeme.

Tumekuwa tukishuhudia mara kadhaa kukosekana kwa huduma ya nishati hiyo na kuzorotesha shughuli za maendeleo. Hali ya kukosekana kwa umeme inatokea kwa kutolewa taarifa mapema ili kupisha matengenezo yaliyopangwa siku na wakati maalumu au kukatika hafla kutokana na hitilafu au maharibiko iwe kwenye gridi kuu ya Taifa ya umeme au eneo maalumu.

Ili kuendeleza shughuli za kila siku za wananchi bila ya kusita, ni lazima ziwepo njia mbadala za upatatikanaji wa nishati ya umeme. Matumizi mbadala yaliyoanza kushika kasi ni ya kutumia nishati ya umeme unaotakana na mwanga wa jua. Nishati hii inasaidia sana linapotokea tatizo la kukatika kwa umeme na hata kwa wananchi wanaoishi kwenye vijiji ambavyo huduma za umeme hazijafika.

### Upatikanaji wa umeme

Jua limekuwa likitumiwa kuzalisha nishati ya umeme yenye uwezo wa kumaliza tatizo la kukatika umeme ambalo ni changamoto kubwa kwa watumiaji wa nishati hiyo. Nishati ya umeme inayotokana na mwanga wa jua ina uwezo wa kuchangia kiwango kikubwa cha umeme katika grid ya taifa kama ilivyo gesi asilia. Aidha, nishati hii ikiunganishwa kwa mfumo wa "automatic redirection", umeme wa kawaida ukikatika, umeme wa jua unajiwasha na kuendelea na matumizi kama kawaida.

Ili huduma ya umeme wa jua ipatikane kwa ufanisi, kunahitajika kuwekwa baadhi ya vifaa hasa kwenye nyumba za biashara na hivyo huepuka kutumia magenereta yenye gharama kubwa kuyaendesha ikilinganishwa na umeme wa kawaida. Katika matumizi ya umeme wa jua, mtumiaji hulazimika kwanza kununua vifaa vitakavyomuwezesha kupata nishati hiyo ili baadaye aweze kutumia umeme kwa muda mrefu bila ya gharama zozote.

Kwa kiwango kikubwa nishati ya umeme unaotokana na mwanga wa jua umeanza

kuonekana ufanisi wake kwani imekuwa ikitumika katika mambo mengi. Miongoni mwa maeneo makubwa yanayotumia umeme huo ni;

### 1. Kwenye taa za kuongozea magari

Mfano halisi unaoweza kutolewa hivi sasa ni matumizi ya nishati hiyo katika taa za kuongozea magari barabarani ambazo kwa kiwango kikubwa zinategemea umeme huo. Faida inayopatikana kwa kutumia taa hizo, ni kwamba mtu anayetembea barabarani hawezi kufahamu iwapo umeme wa kawaida umekatika au la. Kwa hivyo hakuna tatizo la mji kuwa kiza hata kama umeme umekatika.



### 2. Kupasha moto maji

Huduma hii ni muhimu sana hasa katika kipindi cha baridi. Ni wazi huduma hii inayotumia teknolojia ya kisasa inatoa msaada mkubwa wa kufanya maisha ya binadamu kwenda vizuri. Mfano katika vyuo, hospitali, majumbani na taasisi mbalimbali wameweka mfumo huu ambao umekuwa ukileta mafanikio makubwa.

### Vifaa

Viko vifaa maalumu vinavyotumika kwa ajili ya kuunda mfumo wa kupata umeme unaotokana na mwanga wa jua. Vifaa hivyo ni pamoja na "panel", betri, "invertor", "charger controller" na waya.

#### i. "Panel"

"Panel" ni chombo muhimu kinachotumika kwa ajili ya kupata umeme unaotokana na mwanga wa jua. "Panel" ndiyo inayofanya kazi ya kubadilisha mwanga wa jua kuwa nishati ya umeme kwa kutumia seli ambazo ni "silicon". Hiki ni kiungo kikubwa katika mfumo wa kupata umeme wa jua. "Panel" inatakiwa iwe na uwezo mkubwa kuliko betri zinazotumika. Mtu anaweza kuunganisha "panel" hizi kutegemea na matumizi ya umeme anaotaka kuutumia pia kwa upande wa betri anaweza kutumia idadi anayotaka.

#### ii. Betri

Hiki ni kifaa ambacho kina kazi ya kuhifadhi umeme na kutumika wakati ambao jua halipo yaani usiku au muda mwingine kipindi cha mawingu. Inashauriwa "panel" iwe na nguvu kubwa zaidi kuliko nguvu ya betri. Mtu hapaswi kuwa na wasiwasi kuhusu hili kwani nguvu hizo huandikwa kwenye kifaa chenyewe kwa hiyo ni kuangalia maelekezo yaliyotolewa.

#### iii. "Invertor"

"Invertor" ni kifaa kinachotumika kubadilisha aina ya umeme unaozalishwa na "panel" yaani "Direct Current" (DC) kwenda "Alternating Current" (AC) kwa matumizi. Kama tulivyoona kwenye "panel" na betri, hata "invertor" inatakiwa ifanane kiuwezo na betri, lakini ikizidi sio mbaya ingawa isiwe na uwezo mdogo kuliko wa betri.

#### iv. "Charger controller"

Kifaa hichi ni muhimu sana katika mfumo huu kwani hutumika kurekebisha kiwango cha umeme kinachofikia betri. Huzuia ongezeko la umeme na kuzuia kupungua kwa uimara wa betri. Kifaa hichi kinaunganisha kati ya "panel" na betri na "invertor" kwa ajili kuonesha alama kuwa betri imejaa na kinazuia kuendelea betri kuchajiwa pamoja na "panel".

#### v. Waya

Waya zinatumika kwa kuunganisha mzunguko wa umeme kutoka kwenye "panel" kupitia vifaa vyote hadi kwenye matumizi ya mwisho ya mtumiaji. Aidha, kunatakiwa kuweko na uangalifu mkubwa katika uunganishaji kwani taratibu zake za uunganishi ni sawa na zile za umeme wa kawaida. Sheria za uunganishaji ni zile zile kama vile ukubwa wa waya kwenye soketi, swichi, taa, kutoka kwenye "panel", betri na kwengine.

#### vi. Vifaa vyengine

Vifaa vyengine vinavyotumika ni vile vinavyowezesha mfumo kukamilika kama taa, swichi, "socket breaker", "main switch" na vingine vingi vinavyotumika kuunganisha mfumo mzima.

### Tahadhari ya kuchukua

Wakati wa kununua vifaa hivi kuna haja ya kuchukukuliwa tahadhari. Tahadhari hizo ni:

- "Panel" inatakiwa iwe na uwezo wa kuzalisha kiwango cha umeme unachokihitaji kutokana na matumizi.
- Nguvu ya betri isizidi kiwango cha "panel".
- Aina na ukubwa wa waya kutokana na maelekezo ya mtaalamu.
- Kupata ushauri wa mtaalamu kabla ya kununua vifaa hivyo vyote kama "panel".
- Zingatia ubora wa watengenezaji wa vifaa. Ni bora mtu kutumia pesa nyingi kununua vifaa vilivyo bora na vyenye kudumu.

# Ujenzi wa bandari mpya uwekewe kipaumbele

**Ndugu Mhariri,**

Nimesoma kwa furaha Jarida lako lililopita na naomba nitumie fursa hii kwanza kukupongeza kwa dhati kwa kuanzisha Jarida la ZURA. Naamini kabisa kuwa Jarida hili litatumika kama chombo cha Mawasiliano baina ya sisi wananchi na Mamlaka, ambayo inabeba jukumu muhimu kiuchumi na kijamii katika maisha yetu ya kila siku.

Pili, naomba nitumie fursa hii kutoa maoni yangu kuhusiana na huduma za ZURA na zaidi kuhusu mipango ya Serikali ya utoaji huduma za mafuta na gesi.

Nichukue fursa hii kuishukuru Mamlaka hii kwa kuamua kujenga jengo la kisasa maeneo ya Kikwajuni mkabala na viwanja vya Maisara na kuleta sura mpya ya mji kwenye eneo hilo. Hatua hii inaondosha ile tabia iliyokuwa imezoeleka miaka ya nyuma ambapo ofisi za Serikali zilikuwa zikifanya shughuli zao kwenye majengo makongwe yaliyochakaa.

Kwa mara nyengine tena uamuzi wa kujenga jengo hilo unauthibitishia umma kwamba SMZ sio tu imedhamiria kweli kuleta mabadiliko, lakini pia inaonesha kuwa inawezekana Zanzibar kubadilika iwapo kutakuwa na dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko ya kimaendeleo.

Nimefuatilia jitihada za SMZ kupitia ZURA katika kuimarisha sekta ya mafuta na gesi asilia. Takriban mwaka mmoja uliopita nilimshuhudia Waziri anayeshughulikia masuala ya Nishati Bibi Salama Aboud akitia saini mkataba wa utafiti wa uchimbaji wa mafuta na gesi asilia baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Kampuni moja ya Rasulhaimah inayoitwa RAK GAS.

Sherehe za kutia saini Mkataba huo zilihudhuriwa pia na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na kiongozi mmoja kutoka Rasulhaimah. Katika hotuba yake ambayo ilitangazwa moja kwa moja na ZBC TV na Redio, Rais wa Zanzibar alisema faida ya suala hilo isitarajiwe katika muda mfupi ujao kutokana na ukweli kwamba utafiti wa suala hilo unaweza kuchukua zaidi ya miaka saba, kabla ya hatua ya kuchimba mafuta hayo kutekelezwa.

Kwa maoni yangu binafsi, hatua hiyo ni muhimu sana kwa maendeleo yetu na sekta ya mafuta na gesi ambayo ZURA inahusika moja kwa moja. Ingawa suala lenyewe litachelewa, lakini tayari tumelianza na bila ya shaka historia imeshajiandika.

Lakini hatua nyengine ya kufurahisha na kutia moyo ni ule mpango wa Serikali wa kujenga bandari katika kijiji cha Mangapwani kwa ajili ya kushushia mafuta na gesi asilia. Ni dhahiri mpango huo unaweza kuleta tija kubwa kwa nchi kama yetu ya visiwa, ambapo mwelekeo wa uchumi wake unapaswa kuwa wa kutoa huduma zaidi.

Nashawishika sana kuona kwamba hii rai ya pili ya kujenga bandari ndio bora zaidi, sio kwa sababu haitochukua muda kuitekeleza, lakini itatuepusha na mambo mengi ambayo huenda yakatokea katika kipindi cha mchakato wa utafutaji wa mafuta na gesi na vile vile wakati wa kuyachimba hayo mafuta.

Historia inatuonesha kuwa suala la uchimbaji wa mafuta au rasilimali ya mafuta na gesi linakuwa ndio chanzo cha kuleta mifarakano katika baadhi ya nchi duniani. Wananchi wenyewe kwa wenyewe wanagombanishwa ili wafarikiane kwa lengo la kuwapa upenyo wakubwa duniani kugawana rasilimali hizo.

Wananchi wa Zanzibar hivi sasa ni watu wanaopendana sana ukiacha tofauti za kisiasa, ambazo nazo zinazidi kupaliliwa na watu wasioitakia maendeleo nchi yetu kwa maslahi yao binafsi. Lakini hofu nyengine katika hili ni namna ya shughuli yenyewe ya uchimbaji itakavyofanyika.

Itakumbukwa kwamba katika siku za hivi karibuni Zanzibar tumepata mtihani mkubwa katika suala zima la kuchimba mchanga na rasilimali nyengine. Lakini vile vile tumekuwa na hali mbaya katika suala la uhifadhi wa misitu. Kama suala la utafiti limepelekea kutaka kuchafua baadhi ya maeneo ya hifadhi, bado haijafahamika kwa kiasi gani uchimbaji huo utaathiri suala la mazingira hapo mafuta na gesi asilia yatakapopatikana.

Bado ninashawishika zaidi na mpango wa Serikali wa ujenzi wa bandari kwa ajili ya mafuta na gesi sambamba na ujenzi wa matangi makubwa ya kuhifadhia mafuta kwa ajili ya kufanya biashara ya kuyauza kwa nchi jirani. Hii inaweza kuwa biashara nzuri itakayoweza kututoa kwenye umasikini kwa haraka.

Nashauri utafiti ufanyike kwa kuangalia uzoefu wa nchi nyengine zinazofanana na mazingira yetu na kuona lipi lenye manufaa zaidi kati ya biashara ya kuuza mafuta kama wakala au kuchimba mafuta.

**Othman Hassan**
**Mombasa**
**Zanzibar**

# Zanzibar Water Authority (ZAWA)

Let's sustain our clean and safe water
Pay today to see its sustainability.

## Our offices are everywhere to serve our customers

Urban - Madema
Nouth 'A' - Gamba
North 'B' - Mahonda
West 'B' - Kijitoupele
Wete Pemba - Taifu
West "A" - Mwera
Centre Unguja - Koani
South Unguja - Paje
Pemba Chake - Machomane
Mkoani Pemba - Uweleni
Micheweni Pemba - Kilindi

For more information
Contact us:
0774 777 777



# JIEPUSHE NA MAJANGA YA MOTO WA UMEME

Ajali ni tukio linalosababisha madhara yaliyowazi kama vile vifo, ulemavu, uharibifu wa mali pamoja athari nyengine, Ajali ni tukio ambalo hutokezea bila kutarajiwa na kusababisha kubwa au ndogo kwa binadamu. Matukio ya ajali ambayo husababisha madhara madogo kutokana na tahadhari za awali zilizochukuliwa kujikinga na majanga husika.

Baadhi ya waatalamu wanayaelezea matukio yanayoweza kuepukika kuwa sio ajali, wakiamini kwamba ajali ni ile ambayo ni nadra kuepukika na mara nyingi haiwezi kutambulika wala kutabirika. Waswahili wameweka msemo maarufu wa Kiswahili usemao "ajali haina kinga".

Matukio ya moto ambayo wataalamu hawayahusishi na ajali ni mengi na yanatokea mara kwa mara. Uzoefu unaonesha matukio haya hasa katika nyumba za makazi yamekuwa yakisababishwa na hitilafu za umeme au matumizi mabaya ya vifaa vya moto. Kwa kiasi kikubwa inaaminika kwamba matukio ya aina hiyo mara nyingi yanasababishwa na kutokuchukuliwa tahadhari za mapema. Matukio mengi ya moto wa umeme yanaweza kuepukika. Miongoni mwa tahadhari zinazofaa kuchukuliwa katika kujikinga na majanga ya umeme ni pamoja na:

**Kuwa na miundo mbinu imara**

Upo utaratibu unaofahamika kwamba mtu hawezi kuvuta umeme katika jengo ikiwa jengo hilo halijawekewa miundo mbinu ya umeme ambayo kwa mujibu wa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), ni lazima iandaliwe na wataalamu wanaotambulika. Katika kukwepa gharama, watu wengi hutafuta mafundi wa mitaani wasio na ujuzi mkubwa kuweka miundo mbinu hiyo. Ndio maana baadhi ya hitilafu za umeme katika nyumba zinasababishwa na miundo mbinu mibovu ya waya zilizosanifiwa na mafundi wasiokuwa na sifa stahiki.

Katika kupambana na majanga ya moto unaotokana na hitilafu za umeme ni kuhakikisha miundo mbinu ya umeme inaandaliwa na wataalamu mahiri. Majengo nayo wanatakiwa kuwekewa utaratibu kuchunguza na kukagua miundo mbinu hiyo, mara kwa mara. Aidha, waya zibadilishwe kila zinapoonyesha dalili ya kuchoka.

Ni muhimu watumiaji wa umeme kutoa taarifa kwa mtaalamu wa umeme kila wanapobaini hali isiyo ya kawaida katika mfumo wa umeme au ufanyaji wa kazi wa vifaa kama vile mita, switchi, soketi, taa na vifaa vyengine.




## Weka vifaa vya kuhisi moshi (smoke detectors)

Watu wengi hawafahamu kuwa wanaweza kuzuia moto katika nyumba zao kwa kuweka vifaa maalumu vyenye uwezo wa kubaini kuwepo kwa moshi utokanao na moto ndani ya nyumba. Kuna haja ya kuhakikisha kifaa cha kuhisi moshi kinakuwepo kwenye nyumba na kina mfumo wa kutoa mlio ama ishara fulani kumjulisha mhusika juu ya kuwepo kwa tatizo. Hatua za haraka zinafaa kuchukuliwa inapobainika kuna tatizo.

## Vifaa vya kuzimia moto

Kwenye nyumba, vifaa vya kuzimia moto vinahitaji kuwekwa kwenye maeneo mbalimbali kama vile jikoni, varanda na maeneo mengine. Mitungi inayobeba gesi za kuzimia moto ikaguliwe na itunzwe. Kila mtu katika familia afunzwe jinsi ya kutumia vifaa hivi. Inawezekana vifaa hivi visiwe na ufanisi wa kuzima moto mkubwa, lakini vinaweza kutumika kama hatua ya kwanza pale unapobainika moto kabla haujatandaa eneo kubwa.

## Matumizi bora ya soketi na swichi za umeme


Kwenye soketi za umeme na swichi ni miongoni mwa maeneo yanayosababisha moto wa umeme. Hivyo, inashauriwa kufanya yafuatayo

- Epuka kuweka soketi au chanzo chochote cha kutolea umeme chini ya zulia, mikeka au vitu vinavyoweza kushika moto kwa haraka.
- Unapotumia soketi, hakikisha kifaa chako kimeshikilia vizuri kisiwe kinapwaya au kuacha nafasi.
- Usiweke vifaa vingi vya umeme katika eneo moja la soketi.
- Chunguza uimara na usalama wa soketi na swichi mara kwa mara.
- Epuka kuacha soketi na swichi zikiwa zimewashwa kama hazitumiki.
- Epuka kuacha vifaa vikiwa katika soketi kwa muda mrefu hata kama umezima.
- Mwite mtaalamu wa umeme unapohisi kitu kisicho cha kawaida katika ufanyaji kazi wa soketi na swichi zako.

## Vifaa vinavyotoa mwanga

Kuna haja ya kuchukua tahadhari kubwa, mtu anapotumia vifaa vya kutolea mwanga kama vile mishumaa, mwenge na vibatari. Vifaa hivi visiwekwe jirani na vitu vinavyoshika moto kwa haraka kama mikeka, mazulia, vitu vya plastiki, magazeti, mapazia na vinginevyo. Ni kosa kubwa kulala wakati umeacha mshumaa au kibatari kinaendelea kuwaka.

Kuwa makini na vitu vinavyohifadhi mafuta vinavyoweza kulipuka kama vile pikipiki, jenereta na madumu ya mafuta. Ni vyema vitu hivi vihifadhiwe nje ya nyumba.



Itaendelea toleo lijalo

# CRC yapiga hatua licha ya changamoto



Baraza la Kuwawakilisha Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA CRC) limepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yake licha ya kukabiliwa na changamoto nyingi.

Chombo hicho kimeundwa maalumu kwa ajili ya kulinda, kutetea na kusimamia maslahi ya wananchi. Kazi kubwa ya CRC ni kuwashughulikia watumiaji wa huduma za Maji na Nishati, zinazosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishari (ZURA).

Baraza hili la ushauri limeanzishwa Julai 13, 2018 chini ya sheria namba 7 ya 2013 Kifungu 33 cha Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA).

Kwa mujibu wa Sheria hiyo ya ZURA, Baraza limekabidhiwa kutekeleza majukumu muhimu matatu. Majukumu hayo ni:

a. Kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za maji na nishati zinazodhibitiwa na ZURA kwa kutoa maoni, ushauri na taarifa kwa ZURA, Waziri na watoa huduma wa sekta husika.

b. Kupokea na kusambaza taarifa kuhusu maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na ZURA.

c. Kushauriana na sekta husika, Serikali na vikundi vyengine vya watumiaji juu ya masuala yanayohusu watumiaji.

Katika majukumu hayo, CRC inalazimika kuwawakilisha watumiaji maji na nishati katika masuala mbalimbali yakiwemo kwenye mikutano na makongamano ya upangaji wa bei mambo ambayo ni vigumu kwa watumiaji hao kushiriki kwa pamoja.

Mbali na kazi hiyo, baraza linatakiwa kuwahamasisha watumiaji kuweza kushiriki kwenye masuala yanayohusu Maji na Nishati yenye manufaa kwao, kudai haki pindi inapokiukwa na mtoa huduma na pia kulalamikia huduma mbovu na kutoa maoni kwa ajili ya kuimarisha huduma hizo.

Aidha, CRC inapaswa kuwasilisha maoni na ushauri wa mtumiaji kwa watoa huduma, Mdhibiti na Waziri anayehusika na kuhakikisha kuwa malalamiko ya mtumiaji yanashugulikiwa ipasavyo na watoa huduma pamoja na mdhibiti.

Katika kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi, CRC imetayarisha Kanuni za Mwenendo wa Baraza ambazo zinatoa muongozo wa uendeshaji wa vikao vya Baraza na tayari limefanya ziara za kujitambulisha kwa watoa huduma za maji na nishati katika visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na kufanya semina kwa watoa huduma za umeme, maji na ZURA juu ya kuwepo kwake.

Baraza pia limetoa elimu juu ya kuwepo kwake kwa mameneja wa vituo vya mafuta, wauza mafuta na umoja wa madereva wa magari Unguja na Pemba na limeshiriki mafunzo juu ya masuala ya utendaji wa Mabaraza ya Watumiaji yaliyoandaliwa na Jukwaa la Watumiaji Tanzania (Tanzania Consumer Forum).

Katika kutetekeleza majukumu yake, CRC imeweza kushiriki katika vikao vya kutunga kanuni za masuala mbalimbali ya udhibiti vilivyotayarishwa na ZURA kwa lengo la kuwawakilisha watumiaji pia kushiriki katika mikutano inayohusika na upangaji wa bei ya huduma za umeme.

Katika kipindi chake cha utekelezaji, CRC imefanikiwa kujiunga kuwa mjumbe katika Jukwaa la Watumiaji Tanzania (TCF), kushiriki katika maadhimisho ya wiki ya Mtumiaji duniani yaliyofanyika Arusha na kuweza kushauri, kutatua na kufatilia malalamiko kadhaa ya watumiaji wa huduma za maji na umeme.

CRC pia imefanikiwa kutengeneza Kauli mbiu yake isemayo, "sauti yako ndio mafanikio yetu" na kuanzisha Dira, Dhamira na Misingi ya Baraza vitu ambavyo vinatumika kama utambulisho wa Baraza katika shughuli zake.

Pamoja na mafanikio hayo, Baraza limekuwa likikabiliana na changamoto kadhaa, miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kuwepo uelewa mdogo wa wajumbe juu ya kutambua baadhi ya mambo ya kuliendesha Baraza, ugeni wa dhana ya Udhibiti, Utetezi wa watumiaji, Haki na wajibu wa watumiaji kunakosababisha kutokubalika Baraza ipasavyo.

Changamoto nyengine ni Baraza kukosa uwezo wa kulazimisha utekelezaji wa ushauri inaoutoa kwa watoa huduma.

Kuwepo mwitikio na uelewa mdogo wa wananchi juu ya kuwepo kwa Baraza na malengo ya kuanzishwa kwake hali ambayo inasababisha watumiaji kushindwa kulitumia ipasavyo na pia watumiaji kutokuelewa tofauti kati ya shughuli za baraza na ZURA.

Tafauti iliyopo kati ya ZURA na Baraza ni kwamba ZURA inafanya kazi ya kudhibiti huduma za Maji na Nishati ili ziwe bora na Baraza linatoa ushauri kwa ajili ya kuwawakilisha watumiaji katika kulinda na kusimamia maslahi yao.

ZURA ina jukumu la kutoa leseni, kupanga bei, kuweka viwango vya huduma, utatuzi wa malalamiko, kusimamia masharti ya leseni na kutunga miongozo pamoja na kanuni ambapo Baraza lina kazi ya kutoa maoni, ushauri, elimu, kuhamasisha umma, kupokea kero, kuwakilisha na kuunda kamati za watumiaji.




ZURA